**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**

**SHULE YA SEKONDARI WASICHANA SHINYANGA**

**S.L.P 405 SHINYANGA**

Namba za simu:

- Mkuu wa Shule: 0769-770751/0673-770751
- Makamu Mkuu wa Shule: 0764819840
- Matron : 0714010802

Mzazi /Mlezi wa.............................................................................
S.L.P..........................................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WASICHANA SHINYANGA MWAKA -2026**

Ninafurahi kukutarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka……………katika shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga iliyoko Manispaa ya Shinyanga.Hongera sana.

Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe tajwa hapo chini na utapokelewa na Makamu Mkuu wa Shule pamoja na mwalimu wa Zamu.

1. **USAFIRI:**
   Ufikapo mjini Shinyanga kama umeshuka kituo cha mabasi cha Shinyanga (stendi ya Manyoni) panda pikipiki kwenda Soko kuu ambapo utakuta hiace (mabasi madogo) nauli yake ni shilingi 600 ziendazo Old Shinyanga na ushuke kibao kilichoandikwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga.

2. **MAHALI SHULE ILIPO:**
   Shule hii ipo kushoto mwa barabara iendayo Machinjio mpya kilometa 1 kutoka barabara ya lami iendayo Old Shinyanga.

3. **TAREHE YA KUANZA MASOMO:**
   Muhula wa masomo utaanza tarehe ………….. Hivyo utatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………...

**4.MAHITAJI**

**(A)Michango mbalimbali**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | **Mchango wa uendeshaji wa shule** | **65,000/=** |
| 2. | **Tahadhari** | **5,000/=** |
| 3. | **Nembo** | **5,000/=** |
| 4. | **Kitambulisho cha shule** | **5,000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Malipo haya yafanyike kupitia akaunti namba 0150741984500 yenye jina la SHINYANGA WASICHANA SEKONDARI SCHOO.Benki ya CRDB.**

**(B) VIFAA.**

Vifaa vifuatavyo ni lazima mwanafunzi kuja navyo shuleni .

- Godoro (futi 3) upana.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya kuogea na kufulia.
- Mto 1 na foronya za rangi ya pinki zisizo na maua.
- Shuka za kulalia rangi ya pinki 2 , blue bahari 2 na chandarua cha pembe 4
- Nguo za ndani za kutosha na mahitaji yake muhimu.
- Faili la kuhifadhia mitihani yake.
- Vyombo vya kulia chakula (kikombe, sahani, bakuli na kijiko,chupa ya kutunzia making ya kunywa).
- Blanket moja (la kawaida).
- Daftari kubwa 9 (counter books Quire 3), kalamu za wino 30 (blue) ,madaftari madogo dazan 1 na penseli dazan 1
- Mathematical set 1 
- Ream 1 ya A4
- Aje na vitabu vya masomo yake.
- Taulo za kike za kutosha
- Jembe 1 kwa mwanafunzi wa CBG
- Fyekeo 1 na ufagio laini 1 (soft broom ) kwa mwanafunzi wa PCB
- Mopper mbili (2) kwa mwanafunzi wa PCM

**(C)SARE ZA SHULE (UNIFORM):**

- Sketi mbili (2) za draft kama inavyoonekana kwenye kielelezo na ashone rinda box mbele na nyuma ivuke magoti na isiwe na urefu wa kuburuzika kwa ajili ya darasani
- Gauni mbili (2) za dark blue zenye rinda box mbele na nyuma za kushindia ashone mwenyewe. Kitambaa cha Esteem
- Juba/Shungi mbili nyeupe kwa Waislam zinazofunika kifua .
- Shati mbili nyeupe za tetroni, mikono mirefu kwa wakristo.
- Sweta ya ugolo.
- Tai rangi nyeusi.
- Kizibao chenye rangi ya sketi (kama kinavyoonekana kwenye kielelezo.
- T –Shirt yenye kola rangi nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye kisigino kifupi,visiwe vimechongoka mbele na viwe vya kamba jozi mbili.
- Soksi rangi nyeupe ndefu jozi 4.
- Nguo za michezo
  - Track suit rangi ya kijivu nzito (adibas)
  - raba nyeupe za kamba
  - Jezi rangi ya bluu.
  - Skin tight ndefu nyeusi
  - Rain boot nyeusi

**NB: Mwanafunzi ajapo shuleni anatakiwa kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate) Results Slip kidato nne na Bima ya afya kwa ajili ya matibabu.**

**5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

- Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978.

  Unatakiwa kuzingatia (Sheria) mambo ya msingi yafuatayo:.

1) Heshima kwa wazazi, wanafunzi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2) Mahudhurio mazuri katika shughuli zote za kila siku ndani na nje ya shule
3) Kufahamu na Kuzingatia kikamilifu mipaka ya shule na uwepo wa ndani ya mipaka hiyo wakati wote mwanafunzi akiwa shuleni.
4) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
5) Kutunza mali za shule.
6) Kuvaa sare za shule wakati wote, mavazi ya nyummbani hayaruhusiwi shuleni.
7) Kuwahi katika shughuli zote za shule.
8) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9) Kutokuleta radio,simu ya mkononi au card au charger ya simu shuleni, vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari. Mwanafunzi akikutwa na kitu kimojawapo kati ya vitu hivyo adhabu yake ni kufukuzwa shule.
10) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au kumshawishi mwenzake abadili dini wawapo shuleni.
11) Haruhusiwi kutumia mshumaa au kibatari ila ataruhusiwa kumiliki taa inayotumia betri au solar.

7. **MWISHO**.

- Unaporipoti unatakiwa kukabidhi fomu ya ahadi ya mwanafunzi na ahadi ya mzazi/mlezi pamoja na fomu ya uchunguzi wa afya kwa Makamu Mkuu wa Shule.

**KARIBU SANA SHINYANGA WASICHANA SEKONDARI**



**NURAH W KAMUNTU**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli(wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO.**

**MKUU WA SHULE: 0673-770751**
**MAKAMU MKUU WA SHULE:** 0764819840
**MWANDAMIZI TAALUMA:** 0759911957
**MWANDAMIZI MLEZI:** 0735601825

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi

(ii) Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

(vi) Kusuka nywele.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Uvutaji wa sigara

(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja,au kuolewa

(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xi) Kupata mimba.

(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa

(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

(xvii) Kutoroka/kulala nje ya shule bila ruhusa.

**VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI.**

1. FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA(Ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya serikali)
2. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI/MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.
3. FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE.

4. PICHA 2 ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU WA KARIBU NA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA NAMBA ZAO ZA SIMU.

**SHINYANGA MUNICIPAL COUNCIL.**

Shinyanga Girls Secondary School,
P.O.BOX 28,
**SHINYANGA.**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

This form must be completed by a government medical officer.

Student's Full Name............................................................................................ Present age.........................................................Sex:.............................................

Blood test...........................................................Group:........................................

Stool Examination:.............................................................................................
T.S.Test:............................................................................................................ Asthma :............................................................................................................

Eye disorder.......................................................................................................

Nose disorder:...................................................................................................

Ear disorder:......................................................................................................

Skin disease:.......................................................................................................

Anemia :............................................................................................................

Chest :...............................................................................................................
Operations:.........................................................................................................

Serious accidents:.............................................................................................. Any other infection disease:.......................................................................................

Pregnancy:..........................................................................(in case of female)

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defects of impairments chronic of family disease etc.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................

I certify that I have personally examined Mr./Miss...................................................

And found him/her/unfit to pursue further studies.

SIGNATURE...............................

DESIGNATION...........................

(Official rubber stamp)

STATION:..................................

DATE:........................................

**SHULE YA SEKONDARI SHINYANGA WASICHANA.**

**TAARIFA**

**YA MWANAFUNZI**.

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule).

1. Jina kamili:........................................................................................................ Tarehe ya kuzaliwa:....................Wilaya........................Mkoa......................... Taifa :.........................................Dini:..........................................................
2. Jina kamili la baba/mama/mlezi:...................................................................

   Anwani yake:..............................................................................................

   Kazi ya baba/mama/mlezi..............................................................................

   Namba ya simu:..........................................................................................

   **AHADI YA MWANAFUNZI:**

   (a) Mimi.................................................nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya Sekondari Shinyanga Wasichana kuanzia............................hadi nitakapomaliza kidato cha sita.

   (b) Kwa hiyo naahidi kwamba;

   (i) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

   (ii) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kama kushiriki migomo, fujo, makosa ya jinai n.k najua pia SIMU, UTORO na UCHELEWAJI shuleni HAVIKUBALIKI.

   (iii) Nitatunza mali za uuma ambazo ni pamoja na majengo samani, vitabu n.k

Tarehe :..........................................Sahihi ya mwanafunzi.......................................

Sahihi ya Dole gumba [ ]

**AHADI YA MZAZI/MLEZI:**

Mimi:.................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi..........................................Naahidi kwamba;

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za Shule ya Sekondari Shinyanga wasichana iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule.

2. Nitafanya kila niwezalo kumuwezesha mwanangu kusoma kwa kulipa michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Sahihi.....................................................
Tarehe ....................................................



Kitambaa cha sketi






